


MTASK – EAC - FALME MBILI



Mungu akaumba kila kitu katika ulimwengu ambao tunaishi. Kila kitu ambacho alikiumba kilikuwa kizuri.

***Uchore dwara moja kwa upande wa kushoto na uandike “Mungu” ndani yake.**

Katika uumbaji kwake, Mungu aliumba malaika kwenye kumtumikia na kumwabudu. Mmoja wao alitamani kuabudiwa mwenyewe Na aliwadanganya theluthi ya malaika kumfuata yeye na kumwabudu. Mungu ambaye ni Mtakatifu na hawezi kukaa na mwenye dhambi (kuasi kinyume na amri au tabia za Mungu) aliwafukuza wao kutoka mbinguni (Peponi) na aliwaweka nje mpaka siku ya mwisho. Tena, aliumba Jehanamu kwa aliji yao.

***Uchore dwara nyingine ndogo kwa upande wa kulia na uandike “Shetani” ndani yake.**

MTASK – EAC - FALME MBILI

Tukiona falme haya, je, tunaona nini?

Kwa ufalme wa Mungu tunaona kwamba ni UFALME WA NURU

- ➔ Mungu anatawala
 - Watoto wake wanaishi katika UHURU kutoka dhambi na uwezo wa huyu Mwovu (Shetani)
- ➔ Tunaona nini katika tabia za ufalme huu?
 - UPENDO
 - AMANI
 - FURAHA
 - UKWELI

Katika ufalme ya Shetani tunaona ile kinyume. Kwa ukweli, ufalme huu ni YA GIZA.

- ➔ Shetani anatawala
 - Watu wanaishi katika UTUMWA kwenye dhambi na huyu Mwovu (Shetani)
- ➔ Tunaona nini katika tabia za ufalme huu?
 - CHUKI
 - DHIKI
 - HASIRA
 - UDANGAYIFU

Neno la Mungu linatuonyesha kwamba Adama na Hawa walipokula tunda ambalo lilavunja amri ya MUNGU, ile kosa lao, ambalo tunaita DHAMBI lilitutenga Na MUNGU

***Uchore mstari katikati ya madwara**

na kutoka siku ile, sisi sote tumetoka kwenye UFALME WA NURU na kuingia UFALME WA GIZA.

MTASK – EAC - FALME MBILI

***Uchore mstari kutoka dwara la MUNGU mpaka dwara la SHETANI na uandike DHAMBI YA ASILI YA ADAMU BUSTANINI**

Sisi tunastahili MAUTI kwa sababu ya DHAMBI zetu. Kila mtu ambaye ameishi hapa duniani ametenda DHAMBI. Mungu hakufurahi na hali yetu basi aliamua toka siku ile ile kufanya kitusaidia turudi kwa ufalme wake.

Mungu akamtuma YESU MASIHI kwa ajili ya kutengeneza njia kwa sisi ambao tumefungwa katika UTUMWA kuturegesha katika UFALME WA NURU. Huyu YESU MASIHI alifika hapa duniani. Aliishi bila kosa lo lote. Alifundisha na akafanya mambo mengi ya ajabu katika maisha yake. Alishikwa na viongozi wa dini na akauwawa kwa mkono vyao. Baada ya masiku matatu Yesu alifufuka.

Neno la Mungu linatufundisha Yesu alikuwa bila DHAMBI basi aliweza kujitoa kama sadaka kwa ajili ya kulipa ile deni ambayo sisi sote tunayo kama watumwa wa DHAMBI kutununuliwa kutoka UFALME WA GIZA. Kupitia YESU tu, tungeweza kurudi kwa UFALME WA MUNGU.

***Uchore mstari kutoka dwara la SHETANI mpaka dwara la MUNGU Na uandike YESU MASIHI.**

Mungu ametuwezasha kufanya maamuzi. Mtu akiamua kuingia UFALME WA NURU, ataishi mbinguni kwa milele.

***Uandike UZIMA chini ya dwara la MUNGU.**

Mtu akiamua kukaa katika UFALME WA GIZA, atatengwa na Mungu milele. Neno la Mungu linatuambia ya kwamba kitengo hiki kinaitwa MAUTI ya pili.

***Uandike MAUTI chini ya dwara la SHETANI.**

MTASK – EAC - FALME MBILI

Ukitaka kuingia UFALME WA NURU lazima:

- ➔ Ukubali ya kwamba wewe ni mwenye DHAMBI ambaye anaishi katika UFALME WA GIZA
- ➔ Uombe MUNGU akusamehe DHAMBI zako
- ➔ Uamini kwamba YESU ni mwana wa MUNGU na ya kwamba alikufa kwa ajili ya DHAMBI zako msalabani na akazikwa na akafufuka kuonyesha uwezo wake juu ya SHETANI, DHAMBI, na MAUTI.
- ➔ Nyenyekea chini ya mamlaka yake na umruhusu atawale maisha yako na kukufundisha kufuata njia zake.